الجوانب الإيمانية والأخلاقية في الصيام

**HOTUBA YA IJUMAA**

**Pande za kiimani na kimaadili katika funga.**

**Imefasiriwa**

**na**

**profes. Ayman Alasar**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe. Msemaji ndani ya Kitabu chake Kitukufu:

**وَسَارِعُوا إِلَى مَغْفِرَةٍ مِنْ رَبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَاوَاتُ وَالْأَرْضُ أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ * الَّذِينَ يُنْفِقُونَ فِي السَّرَّاءِ وَالضَّرَّاءِ وَالْكَاظِمِينَ الْغَيْظَ وَالْعَافِينَ عَنِ النَّاسِ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ.**

{**Na ukimbilieni msamaha wa Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyo wekwa tayari kwa wacha-Mungu * Ambao hutoa wanapo kuwa na nafasi ya kutoa na wanapo kuwa hawana, na wanajizuia ghadhabu, na wasamehevu kwa watu; na Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema**}.

Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu tu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni Mtume wake na mja wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma na amani pamoja na baraka kwake na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na kwa wale wote wenye kuwafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya utangulizi huo**:

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka Sharia ya ibada ya funga kwa malengo makubwa na hekima, kwani funga ni shule ya imani na maadili mema, mwenye kuzingatia yaliyo ndani ya Quran Tukufu atagundua kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ametaja lengo la ibada ya funga ndani pale aliposema:

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ.**

{**Enyi mlio amini! Mmeandikiwa ibada ya funga, kama waliyoandikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kumcha-Mungu**}. Na kumcha Mungu ndio thamani kubwa ya mambo mema, hivyo imekuja ndani ya Quran Tukufu na kukutana na misingi mbalimbali na kiimani na kimaadili, ambapo Anasema Mola Mtukufu:

**لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ وَآتَى الْمَالَ عَلَى حُبِّهِ ذَوِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَالسَّائِلِينَ وَفِي الرِّقَابِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَآتَى الزَّكَاةَ وَالْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَاهَدُوا وَالصَّابِرِينَ فِي الْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ وَحِينَ الْبَأْسِ أُولَئِكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ .**

{**Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali, kwa kupenda kwake, jamaa na mayatima na masikini na wasafiri, na waombao, na katika ugombozi, na akawa anashika Sala, na akatoa Zaka, na wanaotimiza ahadi zao wanapo ahidi, na wanaovumilia katika shida na madhara na wakati wa vita; hao ndio walio sadikisha, na hao ndio wajilindao**}.

Miongoni mwa pande za kiimani na kimaadili katika funga ni thamani ya kujichunga, kwani funga ni siri kati ya mja na Mola wake, wala hakuna anayefahamu isipokuwa ni Mwenyezi Mungu, nayo ni dalili ya uyakinifu wa mwanadamu ya kufahamika na Mwenyezi Mungu katika hali ya siri au ya wazi, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

**وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُو مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ وَمَا يَعْزُبُ عَنْ رَبِّكَ مِنْ مِثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَلَا أَصْغَرَ مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ.**

{**Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yeyote katika Quran, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo. Na hakifichikani kwa Mola wako Mlezi chenye uzito hata wa chembe katika ardhi na katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa ila kimo katika Kitabu kilicho wazi**}.

Na maana ya usimamizi malipo ya funga yamekuwa na thawabu nyingi hakuna anayefahamu kiwango chake isipokuwa ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambapo anasema Mtume wetu S.A.W:

**كلُّ عملِ ابنِ آدمَ يُضاعفُ، الحسنةُ بعشرِ أمثالِها، إِلَى سَبْعِمائةِ ضِعفٍ، قال اللهُ تعالى: إِلَّا الصَّوْمَ؛ فإنَّه لِي، وَأَنَا أَجْزِي بِهِ، يَدَعُ شَهْوَتَهُ وَطَعَامَهُ مِنْ أَجْلِي.**

"*Matendo yote mema ya mwanadamu yana malipo ya nyongeza, jema moja lina malipo kumi na hufika mpaka mia saba. Mwenyezi Mungu amesema isipokuwa ibada ya funga kwani yenyewe ni yang na Mimi ndiye mlipaji, kwani mfungaji ameacha matamanio yake na chakula chake kwa ajili yangu*".

Na mfungaji ambaye funga yake inasimamiwa na Mola wake basi anapaswa pia kusimamiwa na Mola wake katika matendo yake yote na uzalishaji wake na matendo mengi ya ndani ya mwezi wa Ramadhani na miezi mingie.

Ibada ya funga ni shule ya subira kwa aina zake zote, kwani ndani ya funga kuna kusubiri kukubwa katika kutekeleza utiifu, na kusubiri katika kujiepusha na yaliyo haramu, na kusubiri pia kwenye kujizuia na matamanio, hivyo Mtume wetu S.A.W ameusifu mwezi wa Ramadhani kuwa ni mwezi wa subira, ambapo anasema:

**صَوْمُ شَهْرِ الصَّبْرِ وَثَلَاثَةِ أَيَّامٍ مِنْ كُلِّ شَهْرٍ صَوْمُ الدَّهْرِ.**

"*Funga ya mwezi wa subira (Mwezi wa Ramadhani) na funga ya siku tatu ya kila mwezi ni sawa na funga ya mwaka*" jambo muhimu kwa mfungaji ni pamoja na kujivesha tabia za kusubiri hivyo anapaswa kuondoa chuki na kumsamehe mtu aliyemdhulumu, pamoja na kumpa yule aliyemnyima, na kumfanyia wema aliyemfanyia ubaya, ambapo Mtume SAW anasema:

**وَإِذَا كَانَ يَوْمُ صَوْمِ أَحَدِكُمْ فَلا يَرْفُثْ يَوْمَئِذٍ، وَلاَ يَصْخَبْ، فَإِنْ سَابَّهُ أَحَدٌ أَوْ قَاتَلَهُ، فَلْيَقُلْ: إِنِّي امْرُؤٌ صَائِمٌ.**

"*Siku ambayo mmoja wenu amefunga basi hatakiwi kuongea maneno machafu siku hiyo, ikiwa atatukanwa na yeyote au kumpiga basi na aseme: Mimi nimefunga*".

Kama vile mfungaji wa kweli huwa haongopi wala hafanyi udanganyifu wala hiyana ambapo Mtume SAW anasema:

من لم يدَعْ قولَ الزُّورِ والعملَ بِهِ، فليسَ للَّهِ حاجةٌ بأن يدَعَ طعامَهُ وشرابَهُ.

"*Mtu yeyote asiyeacha kuongopa na kufanyia kazi uwongo wake, basi huyo kwa Mwenyezi Mungu ni kuwa hana haja ya kuacha chakula chake na kinywaji chake*".

****

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe, rehma na amani zimwendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume Muhammad SAW pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Miongoni mwa makusudio muhimu ya funga ni kuhurumiana na hisia ya kibinadamu kwa wanaomzunguka miongoni mwa watu masikini na wenye kuhitaji, hivyo huwasaidia na kuwaliwaza pamoja na kuwafanyia mahitaji yao, kwani Mtume aliwahi kuulizwa ni upi Uislamu bora? Akasema: Kulisha chakula, kutoa salama kwa unayemfahamu na usiye mfahamu.

Ikiwa malipo ya kuhurumiana na wema pamoja na kulisha chakula ni makubwa katika nyakati zengine, basi ndani ya mwezi wa Ramadhani ndio makubwa zaidi, na ni malipo bora ambapo Mtume SAW anasema:

مَنْ فَطَّرَ صَائِمًا كَانَ لَهُ مِثْلُ أَجْرِهِ، مِنْ غَيْرِ أَنْ يَنْقُصَ مِنْ أَجْرِ الصَّائِمِ شَيْءٌ.

"*Mwenye kumfuturisha mwenye kufunga basi ana malipo sawa na malipo ya aliyefuturishwa bila ya kupungua kitu chochote*". Na anasema Abdillah Ibn Abbas R.A: Mtume alikuwa ni mtu bora katika mambo ya kheir na alikuwa mbora zaidi ndani ya mwezi wa Ramadhani.

Ni uzuri ulioje kujifunza kwenye shule hii ya funga masomo ya Kiimani na maadili bora ili tufikie lengo la ibada ya funga na uhalisia wake. Jabir Ibn Abdillah RA anasema: Pindi unapofunga basi na masikio yako yafunge, na ulimi wako ufunge kutokana na kuongopa na kuongea mambo yenye dhambi, na uache kero na maudhi kwa jirani, na uwe na utulivu siku ya kufunga kwako.

Ewe Mwenyezi Mungu ihifadhi nchi yetu ya Misri pamoja na nchi zengine za Kiislamu na Kiarabu.

Aamin.